

MWANAFUNZI WA BIBILIA - 6 Ukombozi



Utangulizi

Ukombozi ni neno la Kiingereza linalotokana na neno la Kilatini lenye maana ya “kununua kitu ambacho kiliwahi kuwa ni mali yako na sasa ni mali ya mtu mwininge”. Hii ina maana ya kukomboa mtu au mali kwa njia ya kulipa fidia. Katika mazingira ya theologia ya Kikristo, Ukombozi maana yake ni kuwekwa huru kutoka kwenye utumwa wa dhambi, na fidia inayolipwa ili kupata huo uhuru. Wazo hilo linalezeze-wa zaidi katika maandiko ya Injili, ambapo Kristo alikuja kuutoa uhai wake kama fidia kwa walio wengi (Mathayo 20:28; Marko 10:45). Mwenye dhambi anaweza kuokolewa kutoka katika kifungo cha Shetani, dhambi na kifo, kwa njia ya damu ya thamani ya Yesu, ambayo ndiyo gharama ya ukombozi. Yesu ndiye *Mkombozi* na pia ndiye fidia ya *ukombozi*.

Katika Agano la Kale

Mkombozi wa aina yoyote – ilikuwa ni maandalizi ya ujio wa Kristo Mkombozi wetu. Kuna sehemu kuu mbili katika jambo hili: kwanza anapaswa kuwa na uwezo wa kulipa gharama yote, na pili anapaswa kutoka katika jamii husika.

Mambo ya Walawi 25:25, 27, 48-49; Ruthu 3:12-13; 4:4-6; Ayubu 19:25;
Zaburi 19:14; Isaya 59:20

Katika Agano la Kale kusudi la Mungu katika ukombozi ni kukomboa kila mtu au taifa na si mtu mmoja tu. Mwanzo wa wazo hili la kwamba ukombozi ni kwa taifa zima ni pale taifa la Israeli walipo kombolewa kutoka katika utumwa wa Misri. Ingawa walikuwa utumwani, Mungu aliwakomboa (Kutoka 6:6; Kumbukumbu la Torati 15:15). Tofauti kuu hapa ni kwamba katika ukombozi huu hakukuwa na malipo yoyote maana Mungu aliwakomboa kwa nguvu zake mwenyewe (Isaya 52:3).

Katika Agano Jipyaa

Hapa tunaona jinsi Yesu anavyotimiza mambo yaliyosemwa katika Agano la Kale. Kwa lugha ya Kiyunani kuna maneno matatu yanayotumika yenye maana ya ‘mkombozi’.

- (a) *agorazo* – kumnunua mtumwa ili aende kwenye soko la watumwa
- (b) *exagorazo* – kumnunua mtumwa ili atoke kwenye soko la utumwa
- (c) *lutroo* – kutoa malipo ya fidia kwaajili ya kumkomboa mtu kutoka katika mauti ya utumwa

Marko 10:45; Luka 1:68; Matendo 20:28; Warumi 3:10, 19, 24; 7:14; 8:2;
1 Wakorintho 1:30; 7:22–24

2Wakorintho 5:14–17; Waefeso 1:7, 14; Wagalatia 3:10; 4:4-5; 1 Timotheo 2:6; Tito 2:14

Gharama au malipo hayo si fedha. Ni damu ya Mkombozi, iliyomwagika kwaajili yetu katika msalaba wa Kalvari. Tumekombolewa kutoka katika mambo matatu.

- Hatia
- Adhabu
- Mamlaka (ya dhambi)

Zaburi **49:15**; Mathayo **20:28**; Yohana **1:29**; 2 Wakorintho **5:21**; Wagalatia **3:13**; 1 Petro **1:18-19**; Ufunuo **5:9**

Nguvu ya msukumo katika ukombozi

Ni upendo wa Mungu. Anayemuamini Yesu atakombolewa kutoka katika utumwa wa dhambi, na atapata neema kutoka kwa Mungu aliye Mkombozi wake. (Tazama Yohana **3:16**)

Hata hivyo kuna masharti matatu ya muhimu yanayo paswa kuzingatiwa. Yule mtu aliyepo chini ya utumwa anapaswa:

- kumuamini Mkombozi wake (Yesu)
- kuamini kuwa malipo yaliyotolewa yanatosha (damu ya Yesu)
- aondoke na kuachana na ule utumwa

Mtumwa aliyekombolewa anapaswa kutokurudi tena katika mazingira ya kuuzwa au kununuliwa.

Zaburi **31:5**; Isaya **43:1**; Yohana **3:18-19; 8:32**; Matendo **8:13, 21-23**; Warumi **6:20-23; 8:2**; Wagalatia **4:31; 5:13**; Waembrania **2:14**

Copyright © Sovereign World Trust, PO Box 777, TONBRIDGE, Kent, TN11 0ZS, UK
www.sovereignworldtrust.org.uk

Publishing and Translation History

First Published in English by Glory to Glory Publications.

Christian Publications International, PO Box 212, Saffron Walden, CB10 2UU - www.christian-publications-int.com
Editor Peter Sammons. Contributors Alex Jacob, David M. Moore, Peter Byron-Davies, Greg Stevenson, Peter Sammons
ISBN English 978-0-9567831-6-5

This Kiswahili translation for Sovereign World Trust by Revd John Y Madinda with permission
Swahili Edition Published by Sovereign World Trust ISBN - Kiswahili 978-1-908010-12-4